

Waziri Ndaki ahamasisha ufugaji kisasa

Berdina Majinge, Mwananchi
bmajinge@mwananchi.co.tz

Iringa. Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki amewataka wafugaji kubadili mbinu ya ufugaji kutoka wa asili wenye kichocheo cha migogoro ya ardhi na kujikita kwenye ufugaji wa kisiasa.

Waziri Ndaki alisema hayo wilayani Mufindi jana, wakati akikabidhi ng'ombe kwa wafugaji wanaonufaika na mradi wa Animal

Gift unaotekelezwa na Shirika la World Vision Tanzania.

Alisema Serikali inatekeleza mpango wa mabadiliko ya sekta ya mifugo nchini, ikiwamo kuhamilisha mifugo kwa kutumia mbegu chotara na kuacha kufuga ng'ombe wengi, badala yake wapunguze idadi ya mifugo.

"Mwaka huu wa fedha tunataka tuhimilishe ng'ombe 373,000 kwa nchi nzima ili hiyo mifugo badala

ya kuzaa ng'ombe wa kienyeji ize ng'ombe machotara watakaokuwa na uzito mkubwa, lakini watakaoweza kutoa maziwa mengi," alisema Waziri Ndaki.

"Tukiendelea kuwa na idadi ya mifuko tuliyonayo sasa hivi tutaeendelea kuwa na migogoro isiyoi-sha kati ya wafugaji na watumiaji wengine wa ardhi."

Waziri alisema kuwa Serikali kwa kushirikiana na Word Vision

watahakikisha wafugaji wana-pewa mbegu na kufundishwa namna ya kufuga kisasa ili waweze kunufaika na mifugo yao.

Kauli hiyo ya waziri ilikuja baada ya mfugaji aliyejitambulisha kwa jina moja la Mgimba kuomba kufundishwa kufuga kisasa kwa kuwa mashamba kwa ajili ya kuan-da malisho wanayo.

Mkurugenzi Mwandamizi wa Shirika la World Vision Tanzania,

Dk Joseph Mayala alisema mradi huo unatarajiwa kutumia Sh1.4 bilioni kwa ajili ya kununua ng'ombe wa kisasa wa maziwa 300, nguruwe 600 na kuku 4,000.

"Tunaomba Serikali iruhusu madume bora 10 yaliyokusudiwa tunayoyahitaji katika mradi huu yanunuliwe katika mashamba ya Serikali ili kuongeza uhakika wa ubora na ufanisi," alisema.